

**MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**22 Novemba, 2016**

**UFAPANUZI WA TAARIFA YA KUPOTOSHA KUHUSU  
MAJI YA “DEW” KUTOKA NIGERIA**

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) imebaini uwepo wa taarifa inayosambazwa kupitia mitandao ya kijamii hususan “WhatsApp” kuhusu uwepo wa maji ya kunywa yaitwayo “Dew” yanayodaiwa kuingizwa kinyemela nchini Tanzania yakitokea nchi ya Nigeria ambako yanadaiwa kuua zaidi ya watu 180 kwa sababu yana sumu ya *Ebola*.
2. TFDA inapenda kuutarifu umma kuwa taarifa hiyo **siyo ya kweli na inapaswa kupuuzwa**.
3. Kwa mantiki hiyo, wananchi wanaaswa kuacha kusambaza taarifa hiyo potofu kwa kuwa haina ukweli wowote na kwamba hapa nchini hakuna maji yaitwayo *DEW* yaliyowahi kuingizwa kutoka nchi ya Nigeria au nchi nyingine yeyote. Ikumbukwe pia kuwa ujumbe huo wa upotoshaji uliwahi kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii miaka ya kati ya 2013 hadi 2014 na kukanushwa na Serikali.
4. Hata hivyo, TFDA inapenda kuujulisha umma wa Tanzania kuwa, imesajili maji ya kunywa yaitwayo “DEW DROP” baada ya kujiridisha kuwa yanazalishwa kwa kuzingatia mifumo bora wa uzalishaji na yanakidhi vigezo vya usalama na ubora. Maji yaliyosajiliwa nchini yanazalishwa na kiwanda cha maji kiitwacho “DEW DROP DRINKS CO. LTD” kilichopo wilaya ya Sumbawanga, mkoa wa Rukwa.
5. Kama ilivyo kwa bidhaa nyingine za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, maji ya kunywa ya “Dew Drop” ambayo yamesajiliwa yamekuwa yalifuatiliwa katika soko kupitia mifumo iliyopo ya udhibiti ili kujiridhisha kuwa yanaendelea kukidhi vigezo vya usalama na ubora kwa lengo la kulinda afya ya mlaji.
6. Wito unatolewa kwa wananchi kuendelea kushirikiana na TFDA katika kutoa taarifa pindi wanapokuwa na mashaka juu ya usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wakati.
7. Kwa maelezo zaidi unaweza kuwasiliana nasi kupitia ofisi za TFDA Makao Makuu zilizopo Mabibo External, Dar es Salaam, Ofisi za Kanda zilizopo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mtwara na Tabora au kupitia barua pepe ya [info@tfda.go.tz](mailto:info@tfda.go.tz).

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Chakula na Dawa**  
**S.L.P 77150**  
**Dar es Salaam**  
[www.tfda.go.tz](http://www.tfda.go.tz)